



## Mabadiliko ya Itikadi za Ujinaishaji katika Jamii ya Wakuria

Roseline Mwikali<sup>a\*</sup>, Ernest Mohochi<sup>b</sup>, James Ogola<sup>c</sup>

<sup>a</sup>Shule ya Elimu, Chuo Kikuu cha Rongo, Rongo, Kenya

<sup>b</sup>Shule ya Elimu, Chuo Kikuu cha Kibabii, Bungoma, Kenya

<sup>c</sup>Shule ya Elimu, Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya

### IKISIRI

Dunia ya leo ya kiutandawazi inawezesha mtagusano wa umma wa kimataifa kidijitali unaoendelea kushuhudia utamaduni chipukizi wa ujinaishaji unaozidi kushika kasi. Hivyo, makala hii inachanganua mabadiliko katika ruwaza za ujinaishaji yanayotokana na athari ya elimu ya magharibi, dini, teknolojia, na utawala katika jamii ya Wakuria pamoja na athari zake. Wakuria ni jamii ndogo ya kundi la Wabantu wa Magharibi inayopatikana katika Kaunti ya Migori nchini Kenya kwenye ujirani na nchi ya Tanzania. Ujinaishaji ni sehemu muhimu ya maisha ya jamii ya Wakuria kwani ni utambulisho wao. Aidha, sawa na jamii nydingine zile, ujinaishaji huwa dafina ya historia yao. Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi mtazamo wa Kihistoria yao *Wodak na Reisgil (2001)* ilikuwa dira katika uchanganuzi wa data zilizokusanya. Data ambayo imetumika katika makala hii ilikusanywa kwa njia ya mahojiano ya ana kwa ana pamoja na majadiliano ya makundi. Idadi ya sampuli ilikuwa watu 42; wa kike 18 na wa kiume 24. Makala hii imebainisha kuwa mabadiliko ya kielimu, kiuchumi, kiteknolojia, kiutowala na kidini yamekuwa na athari kubwa kiitikadi katika ujinaishaji mionganoni mwa Wakuria. Majilio ya elimu ya magharibi, uhuru wa kufanya biashara, mifumo ya kisiasa na mtagusano wa kiteknolojia umepelekeza ukopaji wa majina kutoka makabila mengine nchini Kenya na ulimwenguni kote mionganoni mwa jamii ya Wakuria. Hili linamaanisha kuwa itikadi za ujinsia zilizohodhiwa na kushamirishwa na majina ya kiasili ya Wakuria zinazidi kufifia kila uchao.

### 1. Utangulizi

Wakuria ni kundi la wabantu wanaoishi katika nchi za Kenya na Tanzania. Nchi yao imetangaa kwenye mpaka wa Kenya na Tanzania mashariki mwa Ziwa Viktoria ([Kjerland, 1995](#)). Wakuria ni wakulima wa mifugo hasa ng'ombe na mimea kama vile mtama, mihogo, ulezzi, viazi vitamu, ndizi na mahindi. Aidha, Wakuria ni wawindaji na wafanyibiashara. Shughuli za kila siku hutabakishwa kijinsia kwa mujibu wa itikadi za Wakuria. Itikadi ni mawazo ambayo humwongoza kila mtu ulimwenguni katika kutenda anayotenda, na jinsi anavyotenda na kumsaidia kuamua atekelze yapi, aache yapi, ayatekelze vipi na hivyo kuhalalisha ama kuharamisha matendo anayoyafanya ([Rossiland, 1990](#)).

Katika jamii ya Wakuria zipo shughuli za jinsia ya kiume na za jinsia ya kike kama inavyoolekezwa na itikadi za ujinsia. Itikadi za ujinsia ni imani, mielekeo na mitazamo inayoongoza jamii kuhusu mgawanyo wa majukumu kwa kuangalia jinsia. Mionganoni mwa mambo yanayodhihirisha mgawanyo wa majukumu katika jamii

### KUHUSU MAKALA

*Maneno Muhimu:*

Ujinaishaji,  
Itikadi,  
Nadharia,  
Wakuria,

*Historia ya Makala:*

Tarehe ya Kutumwa: 16 Septemba 2024  
Tarehe ya Kurekebishwa: 30 Oktoba 2024  
Tarehe ya Kukubalika: 05 Novemba 2024  
Mtandaoni: 27 Novemba 2024

hi ya Wakuria ni majina wanayopewa wanajamii. Hili linamaanisha kuwa itikadi ni sehemu muhimu inayochangia katika kuelewa jamii kikamilifu. [Holmes & Meyerhoff \(2003\)](#) na [Allagbe \(2016\)](#) wanashadidia kuwa majina ya wanajamii huweza kuelekeza jinsi wanajamii huuona ulimwengu wao kitamaduni, kiitikadi na matukio ya kihistoria katika maisha yao. Kwamba, ruwaza za majina hutambulisha jinsi wanajamii hujichukulia na kuwachukulia wengine, hueleza historia yao, desturi zao na vile vile huweza kutambua kile wanajamii hupenda sana.

Ujinaishaji ni mbinu ya kutoa majina. Kama aelezavyo [Essien \(1986\)](#) ujinaishaji ni shughuli ya kiakili, kihisia, kiisimu na kitamaduni na kwamba kupitia majina utambulisho wa jamii na muundo wa lugha yake huweza kubainika. Ujinaishaji ni mchakato wa kuwakilisha mikataba ya kiitikadi au kujenga mfumo wa kiimani. Hivyo basi, kila jamii huwa na mbinu tofauti na za kipekee za kutoa majina kwa watu wake, wanyamapori, mifugo na sehemu mionganoni mwa vitu vingine

\* Mwandishi Mkuu. Simu: +254716214626; Barua Pepe: [rosekasuma@yahoo.com](mailto:rosekasuma@yahoo.com)

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kenya.

Nukuu: Roseline M., Ernest M., & James O. (2024). Mabadiliko ya Itikadi za Ujinaishaji katika Jamii ya Wakuria. Jarida la Kiswahili Sanifu 1 (2024), 18 – 25.

vinavyoizunguka. Tofauti hizi hazijitokezi katika majina tu bali pia, katika maana inayosimbwa katika majina hayo. Majina kama kipashio muhimu cha lugha huwa ni sehemu ya utamaduni wa jamii na kila jamii hutumia lugha yao kueleza au kubainisha "ulimwengu" wao, ulimwengu ambaو hudihihirika katika mwenendo wa maisha yao. Kwa miongo michache iliyopita kumekuwa na uchipuzi wa ruwaza mpya katika jamii ya Wakuria. Uchipuzi huu unatokana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kama inavyojadiliwa katika makala hii.

## 2. Mbinu Za Utafiti

Utafiti ulifanyika ulikuwa wa kiuthamano na ulifanyika katika kaunti ya Migori nchini Kenya mwaka 2020, idadilengwa ikiwa ni wanajamii Wakuria wanaoishi katika kaunti ndogo za Ntimaru, Kuria Mashariki, Kuria Magharibi na Maabera. Sampuli iliyotumika iliteuliwa kimaksudi na kimapokezano. Data ilikusanya kwa kutumia mahojiano na majadiliano ya makundi. Jumla ya watafiti wa 42 walihojiwa ana kwa ana 24 wakiwa wa jinsia ya kiume na 18 wa jinsia ya kike. Aidha, majadiliano ya makundi yalifanyika manne, mawili kwa kila jinsia. Kila kundi lilikuwa na watu wanane. Mwongozo wa usaili ulitumika katika mahojiano na vile vile majadiliano ya makundi ilikukusanya data. Katika uchanganuzi, ni majina ya asili yaliyosheheni itikadi za ujinsia yalizingatiwa.

## 3. Msingi wa nadharia

Mjadala katika makala hii umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi (UHU) mtazamo wa Kihistoria. Nadharia ya UHU iliasisiwa mwanzoni mwa karne ya 19 huko Amsterdam. Nadhadria hii iliasisiwa na Ruth Wodak. Wengine waliokuwa muhimu katika kuchangia nadharia hii walikuwa: Teun Van Dijk, Norman Fairclough, Gunther Kress, Thee Van Leeuwen. Nadharia hii ilitumika kuchunguza jinsi matumizi mabaya ya mamlaka ya kijamii na ukosefu wa usawa miongoni mwa wanajamii huhalalishwa, hushamirishwa na/au kупингwa kupitia kwa usemi (Dijk, 2001). Uchanganuzi wao ultambua dhima ya lugha katika kuunda mahusiano ya kiuwezo.

Kazi hii imetumia nadharia ya UHU mkabala wa Usemi Kihistoria, kueleza jinsi mahusiano ya kijinsia hujengwa kufuatia mpangilio maalum katika jamii ya Wakuria kwa kuzingatia data iliyopo ya miktadha ya sasa na ya kale. Uchanganuzi hakiki Mtazamo wa Kihistoria hulenga kuhakiki usemi kwa kuzingatia mitazamo mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kihistoria. Hususan, namna mitazamo hii husimbwa katika ishara na vipashio vya lugha. Waasisi wa mtazamo huu (Wodak & Reisgl, 2001) hushadidia dhana, mawazo, msimamo na kategoria zilizopendekezwa na Van Djik (Kujisawiri kwa njia chanya ilhali, unasawiri wengine kwa njia hasi). Kwa mujibu wa Huckins (1997) Uchanganuzi Hakiki wa Usemi Mtazamo wa Kihistoria huwa na mihimili mitano lakini mjadala katika makala hii uteangozwa na mhimili wa kintazamo. Mhimili huu ulikuwa dira katika kubainisha ruwaza za ujinaishaji katika jamii ya Wakuria, kwamba wanawake hupewa majina yepi na wanaume hupewa yepi. Aidha, mhimili huu ulikuwa dira katika kufafanua

jinsi majina haya huchangia kuendeleza ujaamiishaji wa msichana au mvulana na majukumu yake andamizi.

## 4. Matokeo na Majadiliano

### 4.1. Mabadiliko katika Ujinaishaji

Majilio ya dini za kigeni, elimu, na teknolojia yamechangia kwa kiasi kikubwa mabadiliko katika shughuli ya ujinaishaji katika jamii nyngi ulimwenguni. Tibezi na wenzake (2021) anaeleza kuwa huko Ulaya katika karne ya 18 na 19 kulishuhudiwa mabadiliko kwa kasi katika uteuzi wa majina. Anaeleza kuwa wazazi wengi huko Concord, Massachusetts waliwapa mmoja wa watoto wao jina la kwanza au jina la Kibiblia lakini baadaye tamaduni hii ilipungua sana. Matumizi ya majina ya babu na bibi kwa watoto ya lipungua.

Neethling naye katika Moyo (2010) aliangazia mabadiliko ya ujinaishaji kihistoria - kabla na baada ya uhuru katika nchi ya Afrika Kusini. Katika utafiti wake alibainisha kuwa majilio ya Wakristo yalileta maendeleo kwani watoto wa Xhosa walipewa majina mapya kanisani na shulen. Majina haya yaliitwa ya "kanisa" au ya "shule." Aidha, nchini Malawi mabadiliko haya yalishuhudiwa huku yakihuushwa na ukoloni. Hii ni kwa sababu wamisheni ndio waliwatangulia wakoloni wa Uingereza kwa minajili ya maandalizi. Moyo (keshatajwa) anaelezakuwa Malawi nanchi za Afrika kusini, Waafrika weusi walipewa majina mapya ya Kiingereza. Sababu ya mabadiliko haya ilikuwa wakoloni hawakuweza kutamka majina ya Kiafrika na pia waliyahusisha na dhambi, giza na hali ya kuwa nyuma kimaendeleo (Macheba, 2002). Majina haya mapya yalionekana kufaa katika mazingira mapya ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Ujinaishaji katika jamii ya Wakuria umedhihirisha mchomozo wa mabadiliko ya kasi kutokana na ujio wa elimu, dini za magharibi na teknolojia. Wanajamii wanatumia ruwaza za ujinaishaji ambazo hazijikiti katika itikadi za jamii ya Wakuria. Makala huu inajadili matokeo ya mahojiano ya ana kwa ana na majadiliano ya makundi yalifanyika katika jamii hii kuhusu mabadiliko katika ujinaishaji na athari zake.

### 4.2. Mabadilikoyaliyotokananaelimu

Kwa mujibu wa wasailiwa, kabla ya majilio ya elimu ya kimagharibi, jamii ya Wakuria ilikuwa na elimu yao, elimu ya kijamii ambayo iliendeshwa kwa misingi ya itikadi zilizo tawala ama jinsia ya kiume au ya kike. Mwita (2005) anaeleza kuwa elimu hii, wanajamii walifunza na kusisitiziwa maadili, majukumu, mielekeo na matarajio ya jamii mintarafu ya mihimili ya itikadi na utambulisho wao. Aidha, elimu ilitolewa kwa kutegemea rika la kila mwanajamii. Walimu vile vile walikuwa mahususi. Mathalani, watotowa kike walifunza na kina bibi ambaو hudihihirika katika masuala mbalimbali ya kitamaduni na kuitikadi kuhusu jinsia ya kike na watoto wa kiume walifunza na kina babu ambaو nao walikuwa na tajriba pana kuhusu utamaduni na itikadi za jamii ya Wakuria.

Utafiti huu ulibaini kuwa dini ndiyo ilitangulia katika jamii ya Wakuria kisha elimu ya magharibi. Shule za

kwanza zilijengwa kulikokuwa kumejengwa makanisa kwani wamisheni waliojenga makanisa haya ndio walifadhili ujenzi wa shule hizo pamoja na mchakato wa utoaji elimu yenye. Hata hivyo, jamii ya Wakuria haikupokea elimu hii kwa mikono miwili. Wasailiwa walieleza kuwa jamii iliiona elimu hii kama mbini iliyotumiwa na wazungu kuwapokonya na kudumaza utamaduni wao. Kwa hivyo, watoto wa kiume tu ndio walioruhusiwa kwenda shulen. Hata hivyo, sio watoto wote wa kiume walioruhusiwa kwenda shulen bali ni wale tu walioonekana kuwa dhaifu na wanyonge.

Watoto walioonekana kuwa na nguvu na shupavu hasa katika shughuli za kulisha ng'ombe hawakuruhusiwa katu kuuona mlango wa darasa. Hii ni kwa sababu shule ilionekana kukinzana na itikadi za jamii katika kumkuza mtoto wa kiume kuwa shujaa na aliye na uwezo wa kuwalinda ng'ombe. Kwa minajili hii, wanyonge ndio waliruhusiwa kwenda shule. Pamoja na haya, mzee aliywapeleka watoto wake wa kiume shule alizomewa sana na wazee wengine katika jamii kwamba aliwaacha wanawe waende shule huku wakiacha mifugo bila mchungaji.

Makundi mbalimbali ya wamishenari; Waroma, Wasabato, PEFA na Maranatha walijitahidi kukuza elimu lakini jitihada zao mara nyangi ziliambulia patupu. Wengi wa wanafunzi hawa walienda shulen kwa siku zisizozidi saba kisha kuacha na kurudi kushiriki katika shughuli mbalimbali za nyumbani hususan kuwapeleka ng'ombe malishoni. Hata hivyo, wengi waliopolekwa shulen walikuwa wamekomaa. Waliofaulu kuendelea walisoma darasa moja kwa muhula mmoja kisha kusogezwa kwenye darasa jingine. Msailiwa mmoja alituarifu kuwa alisoma darasa la kwanza hadi la nne ndani ya mwaka mmoja kwa kuwa alikuwa mwerevu.

Ilikuwa mwiko kwa mtoto wa jinsia ya kike kwenda shulen. Mosi, wanawake hawakuruhusiwa kutoka nyumbani na pili wao walikuwa wageni kwani walitarajiwa kuozwa na kuiletea familia yao malii. Ujio wa elimu umeweza kuibua mabadiliko yenyehaja ya kutajwa katika ulingo wa ujinaishaji katika jamii ya Wakuria kama ifuatavyo.

#### **4.2.1. Mabadiliko ya muundo wa Majina.**

Wengi waliopata nafasi ya kwenda shulen hawakutaka kujinasibisha na wale ambaa hawakuwa wameuona mwanga wa elimu. Ili kuonyesha tofauti yao, wasomi walichopeka sauti ngeni katika majina yao. Mabadiliko haya yakawa ya kiothografia. Wakati jina liliandikwa kwenye vyeti vya kuzaliwa, kitambulisho cha taifa au nyaraka za shulen tofauti hii iliweza kudhihirika. Hata hivyo wapo wengine ambaa walitaka kudumisha asili yao, hivi kwamba hawakuwa tayari kukengeuka. Katika utafiti wetu ilibainika kuwa jinsia ya kike ndiyo ilitekwa na ukengeushi huu kwa asilimia kubwa ikilinganishwa na jinsia ya kiume. Sababu kuu ilikuwa ni kutaka kuonyesha jamii yao kuwa wao walikuwa viumbe tofauti waliojua haki zao kama walivyo kuwa wamefunzwa shulen. Hii ilikuwa njia moja ya kuonyesha jamii walimoza liwa kuwa wao wamejitanzia kutoka kwenye minyororo iliowafunga

wanawake wenza jikoni na katika masuala ya uzazi. Mifano ya majina yaliyobadilishwa yapo katika **Jed. 1**.

**Jed. 1:** Majina yaliyobadilishwa kimuundo. Asili: Nyanjani, 2020

Jina asilia	Jina jipya	Sauti iliyochopekwa
Gati	Ghati	/h/
Boke	Bhoke	/h/
Robi	Rhobi	/h/

Mabadiliko haya pia yalidhihirika pale ambapo mtoto alikuwa amepewa jina la babu au bibi kisha alipoenda shulen akababilisha muundo wa jina lake ama kwa kujua au kutojua kama katika **Jed. 2**.

**Jed. 2:** Majina yaliyobadilishwa kimuundo. Asili: Nyanjani, 2020

Jina asili	Jina jipya	Sauti iliyochopekwa
Boke	Bowke	/w/
Boke	Bowkey	/w/ na /y/
Mwita	Mwieta	/e/
Mwita	Mwyter	/y/, /e/ na /r/
Machera	Mercherah	/e/, /r/ na /h/
Mogesi	Mogezi	/z/

Wasailiwa walitaja kuwa watoto hawakutaka kuhusishwa na ukale wa jamaa waliopewa majina yao pamoja na itikadi zilizoendelezwa na majina hayo. Walitaka kuonekana na kusikika tofauti na akina babu na bibi. Tofauti hii ilikuwa ni kuchopeka sauti za lugha ya Kiingereza katika majina yao.

#### **4.2.2. Majina ya wasomi na watu maarufu kupendeleva.**

Pamoja na kuwa dini na elimu ziliambatana katika jamii ya Wakuria, dini ilitangulia katika kubadilisha itikadi za ujinaishaji katika jamii hii. Mmoja wa wasailiwa alieleza kuwa wanajamii walipewa majina ya kikristo kuashiria kuwa wao walikuwa viumbe wapya, ambaa hawakufungwa na itikadi za kale za jamii yao. Itikadi hizi zilihusishwa na giza na upumbavu. Kadri walivyoenda shulen mtazamo wa majina ya kikristo ambayo yalitolewa kwenye biblia ulibadilika. Sababu tulizopata ni kuwa, majina haya yalihusishwa na ukale na kizazi kilichoelimika kikawa kinayaona kuwa yamezeeka. **Jed. 3** linaonyesha mifano ya majina haya.

**Jed. 3:** Majina yaliyotokana na watu maarufu. Asili: Nyanjani, 2020

Jina	Asili
Wayne	Mchezaji kambumbu
Rooney	Mchezaji kambumbu
Celine	Mwanamuziki
Jeneffer	Mwanamuziki
Jefferson	Kiongozi wa Marekani

Pili, baadhi ya jamaa waliokuwa wamebatizwa waliasi baadaye. Baada ya kuasi wakarudia au wakaanza maisha yaliyokuwa kinyume na matarajio ya jamii ya wakristo na wasomi kama vile ulevi na kuo wake wengi. Kwa sababu hizi wanajamii walikataa kuwapa watoto wao majina ya waasi hawa kwa kuhofia kuwa wana wao wangerithi tabia hizi za uasi. Ndiposa watoto hupewa majina ya watu maarufu katika taaluma mbalimbali au usanii. Mifano ya majina tuliyopata yameonyeshwa katika **Jed. 3**.

#### **4.2.3. Ufupisho wa majina**

Ujio wa elimu ulipelekea majina ya wanajamii wengi kufupishwa. Kwa mujibu wawasailiwa wetu, ufupisho

huu ulikuwa njia mojawapo ya wahusika kujitambulisha na usasa mintarafu ya maendeleo na mabadiliko katika jamii. Kama ilivyokuwa itikadi ya ujinaishaji, mtoto alipewa jina la jamaa aliyeaga ili kumuenzi. Watoto hawa walipoenda shule waliyababalishi majina haya kwa kuyafupisha. Mifano ipo katika **Jed. 4:**

<b>Jed. 4:</b> Majina yaliyofupishwa. Asili: Nyanjani, 2020		
Jina Asili	Jina Jipyä	Jinsia
Stephen	Steve	Kiume
Abednego	Abed	Kiume
Marcela	Cela	Kike
Celina	Lina	Kike
Caroline	Carol	Kike

Hisia za wasailiwa zilikuwa kuwa wanaofupisha majina yao huwa wanajaribu kukataa itikadi zilizokuwa zinaendelezwu na majina haya kupitia warejelewa. Kwa kuwa walikuwa wamesoma na kuwa na mtazamo mpya kuhusu maisha hawakutaka tena kuhushishwa na majina haya ya kale yaliyokuwa na itikadi za kale. Hata hivyo, ufupisho ambao ulionekana kuenea kwa upana ulijitekeza sana katika majina ya kike. Jina la kike lilitofupishwa lilitumika na wanajamii wote kumrejelea mhusika ikilinganishwa na la kiume ambalo lilitumika mara nyingina rika lake pekee.

#### 4.2.4. Mifanyiko ya Kifonolojia katika Majina yenyé asili ya Kigeni.

Lugha inapoingiza maneno yenyé asili ya kigeni kwenye mfumo wake, utohozi wa kifonolojia hutumika ili maneno hayo yaafikiane na kuendana na muundo wa lughahopeksi/kopaji. Utohozi huu hutekelezwa kupitia kwa mifanyiko mbalimbali ya kifonolojia mathalani, udondoshaji, uchopekaji na uimarisaji wa fonimu. Utafiti huu ulijihuisha na lugha ya Kikuria hasa majina kama aina ya maneno katika lugha hiyo. Mifanyiko ya kifonolojia iliyojitekeza katika baadhi ya majina yaliyokopwa kutoka lugha nyingine ni pamoja na; Udondoshaji na *Uchopekaji*. Mifano katika **Jed. 5:**

**Jed. 5:** Jina likiwa na konsonanti mbili mtawalia. Asili: Nyanjani, 2020

Jina la kigeni	Jinsia	Baadayamfanyiko	Ainayamfanyiko
Gregory	Kiume	Girigori	Uchopekaji /i/ na udondoshaji /e,y/
Bridgit	Kike	Birigita	Uchopekaji /i,a/ na udondoshaji /d/
Martha	Kike	Marita	Uchopekaji /i/ na udondoshaji /r,h/
Charles	Kiume	Charisi	Uchopekaji /i/ na udondoshaji /l,e/
Margaret	Kike	Magarita	Uchopekaji /a/, udondoshaji/r/, huimarisaji /e-i/

Kanuni ya udondoshaji huhusu kuachwa kwa sauti fulani katika matamshi wakati fonimu mbili zinapabiliana. Kwamba, katika mazingira hayo sauti ambayo hapo awali ilikuwepo hutoweka (*Kihore na wengine*, 2010). Kwa hiyo, udondoshaji ni hali ya

kuondoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi au neno. Mfanyiko wa udondoshaji katika jamii ya Wakuria unadhihirika katika utohozi wa majina yenyé asili ya Kiingereza pale ambapo kipashio fulani cha neno husika kinatoweka au kudondoshwa kabisa katika mazingira maalum ya kifonolojia au ya kimofolojia (*Buliba*, 2010). Udondoshaji kwa hivyo unahuhsisha irabu, konsonanti na hata silabi. Data ya utafiti huu ilidhihirisha udondoshaji kama ifuatavyo;

Mifano hii vile vile inaonyesha kuwa pale ambapo konsonanti ilidondoshwa palichopekwa irabu kwa minajili ya kuuafiki mfumo asili wa lugha ya Kikuria wa uundaji wa maneno. Uchopekaji hurejelea uingizaji wa sauti moja au zaidi katika neno (*Habwe & Karanja*, 2004).

**Jed. 6:** Sauti za kigeni zilidondoshwa na zile za asili kuchopekwa. Asili: Nyanjani, 2020

Jina la kigeni	Jinsia	Baada ya mfanyiko	Aina ya mfanyiko
Colleta	Kike	Koreeta	Uchopekaji wa irabu /e/
Siprine	Kike	Sibirina	Uchopekaji wa irabu /i/
Joseph	Kiume	Yesebu	Uchopekaji wa irabu /e/
Rael	Kike	Raeri	Uchopekaji wa irabu /i/
Daniel	Kiume	Tanieli	Uchopekaji wa irabu /i/
Catherine	Kike	Katarina	Uchopekaji wa irabu /a/
George	Kiume	Choochi	Uchopekaji wa irabu /o/
Josephine	Kike	Yosebina	Uchopekaji wa irabu /a/
Enock	Kiume	Noka	Uchopekaji wa irabu /a/

Kutokana na data katika **Jed. 6**, utafiti wetu ulibaini kuwa kuna baadhi ya sauti ambazo zipo katika lugha geni (chasilii) mathalani: /c/, /l/, /d/, /p/, na /j/ ambazo hazipo katika lugha ya Kikuria. Katika mchakato wa ukopaji na utohozi wa majina, sauti hizo hupewa visawe vyake kutokana na namna sauti husika inavyotamkwa na pia inavyosikika katika utamkaji mathalani: /k/, /r/, /t/, /bh/, na /ʃ/ mtawalia. Mifanyiko hii ilipelekea kuundwa kwa silabi zenyé uasili zaidi mintarafu ya muundo asilia wa lugha ya Kikuria. Kwa hali hii kama utafiti wetu uliyobaini wasailiwa wengi hawakuweza kutambua kuwa majina haya yalikuwa yenyé asili ya kigeni kwa jinsi yaliyokuwa yamesawazishwa na kufanywa yafumane vizuri na majina yale ya kiasili.

#### 4.2.5. Matumizi ya teknolojia ya kidijitali

Kupitia teknolojia ya kidijitali, wasailiwa walieleza kuwa wazazi huweza kujua sifa zinazoambatana na jina wanilotaka kumpa mtoto. Mathalani, wapo wazazi ambao wamewapa watoto wao majina yenyé mianzo ya sauti sawa, kwa mfano tulipata katika familia tatu watoto wenye majina yafuatayo:

- i. Bahati, Baraka.
- ii. Vicky, Vinny.
- iii. Sofia, Stella, Skyllar.

Matumizi ya teknolojia ya kidijitali iliwasaidia Wakuria kujua sifa zinazoambatana na jina walilotaka kumpa mtoto. Aidha waliweza kujua tafsiri ya majina haya. Mifano ya majina katika **Jed. 7:**

**Jed. 7:** Tafsiri ya majina na maana yake

Kiingereza	Kiswahili	Jinsia	Maana
John	Yohana	Kiume	Mungu ni mwenye neema.
Samwel	Samweli	Kiume	Mungu amesikia.
Grace	Neema	Kike	Nimependelewa.
Irene	Irini	Kike	Amani.

#### 4.2.6. Uhulutishaji

Uhulutishaji ni mbinu ambapo maneno ambatani huundwa kutokana na sehemu fulani za maneno mengine ([Mweri, 2011](#)). Utafiti huu ulibaini kuwa wazazi wengi walitumia uhulutishaji katika kupata majina ya watoto wao. Walieleza kuwa hawakutaka jina ambalo liliashiria asili ya mtoto wao au kuambatana na itikadi zozote. Mtoto wa kwanza ambaye katika jamii ya Wakuria ana jina mahususi, alipewa jina lililohulutishwa kwa kutumia majina ya kigeni ya wazazi wake. Mathalani,

Vincent + Dorothy - Vinthy.

Moses + Ann - Monn.

#### 4.2.7. Tafsiri ya ruwaza za ujinaishaji.

Wasailiwa walieleza kuwa wapo wazazi waliweza kutafsiri ruwaza za ujinaishaji katika Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo, Kiswahili kilitumika sana kutokana na mtagusano wa jamii hii na majirani wao Watanzania ambao lugha yao ya kwanza huwa Kiswahili. Mfano wa tafsiri hizi ni katika [Jed. 8](#).

**Jed. 8:** Majina yaliyotafsiriwa. Asili: Nyanjani, 2020

Ruwaza	Jinaasili	Tafsiri
Kifunguamimba wa kiume	Chacha	Mshindi
Baba kuwa safarini	Mogendi	Safari

#### 4.2.8. Vitabu

Ilibainika kuwa wazazi wengi waliwapa watoto wao majina ambayo yalitokana na wahusika katika kazi za fasihi walizokuwa wamezisoma. Mfano wa majina haya yalikuwa Chausiku, Hidaya, Rehema, Bahatina Subira. Mengi ya majina haya yalikuwa ya kike. Kwa mujibu wa wasailiwa, mabadiliko haya yaliashiria kuwa wahusika walikuwa hawataki kuhusishwa na itikadi zilizokuwa zinaendelezwa na majina yale ya asili na kwa maana hiyo kuwapa watoto wao majina ambayo hayataziendeza itikadi hizo.

#### 4.2.9. Utawala

Kabla ya majilio ya mkoloni, Wakuria waliishi kama jamii moja. Msailiwa alitureleza kuwa Mwirege angetembea kutoka Bwirege hadi Bugumbe na alipochoka alilala njiani kwa Wakira au Wanyabasi. Hakuna aliyeongoza ukoo kwa misingi ya kuwatenganisha Wakuria. Wengine walieleza kuwa wakoloni hawa ndio walileta mipaka baina yao. Baada ya wao kuondoka, viongozi walioshika hatamu wakaliendeza suala hili la mipaka na utambulisho wa kiukoo hasa ya koo zote nne ili kujiendeza kisiasa na kiutawala. Katika mabadiliko haya yote, yapo yaliyogusa ujinaishaji.

Wasailiwa walieleza kuwa yapo majina yanayoashiria majilio ya siasa katika jamii ya Wakuria. Kilichobainika ni kuwa Wakuria walikuwa wahafidhina, hivi kwamba walishikilia kindakindaki mila, desturi na itikadi zao. Hawakupenda kamwe kukopa majina mageni yoyote kutoka nje ya jamii yao. Ilipowalazimu kukopa jina kutoka nje, maadili na sifa andamizi za mwenye jina yalipewa kipaumbele. Kwa minajili hii ni majina ya watu waliotambulika kwa upana kuwa mashujaa tu ambayo yaliweza kupewa watoto wa Wakuria. Majina haya pia huweza kubashiri kipindi ambacho alizaliwa mtoto. Mathalani katika [Jed. 9](#).

**Jed. 9:** Majina yaliyotokana na tawala mbalimbali. Asili: Nyanjani, 2020

Kenyatta	Enzi za Rais hayati Mzee Jomo Kenyatta
Kimanzi	Enzi za shujaa Dedan Kimathi
Thomas	Enzi za Thomas Mboya
Beneti	Aina ya kisu kirefu kilichotumika wakati wa vita ya kikoloni

Jamii ya Wakuria haina sauti /th/ na ndiyo maana kupidia mifanyiko ya kifonolojia jina Kimathi libibadilishwa na kuwa Kimanzi. Kwa upande wa jina Beneti, wasailiwa walieleza kuwa baadhi ya wanaume Wakuria walihusika katika vita ya mkoloni. Kabla ya hapa walihusika kwenye Vita vya Kwanza vya Dunia. Kwenye Vita hivi, Mkuria (Mnyabasi) aliuu adui kwa kutumia silaha hii. Ili kuituliza miungu ya mwendazake isije ikamwandama kulingana na itikadi za jamii ya Wakuria, ilimbidi amwite mtoto wake wa kiume Beneti kwa maana kwamba kisu hiki ndicho kilimwua yule mkoloni wala si ye - Mkuria. Jina hili liliendezeza itikadi kuwa vita ni shughuli ya kiume na huhitaji ushupavu.

Majina haya yalikuwa ya jinsia ya kiume tu. Aidha ilibainika kuwa japo Wakuria walitangamana na wakoloni - Wajerumani (Tanzania) hawakukopa jina lolote kutoka kwao. Wapo wengine ambaa walishiriki katika Vita ya Kwanza ya Dunia lakini hakuna majina mageni yaliyotokana na matukio haya. Sababu iliyopatikana ni kuwa Wakuria walichukia unyanyasaji na mauaji, masuala yaliyohusishwa na wakoloni na hivyo wakachukia majina yao pia.

Kutokana na utawala huu ilishadidiwa kuwa utawala ni sababu tosha na muhimu ya kupelekeea lugha kuathiriana na hivyo kufifisha itikadi za jamii husika. Lugha ya Kikuria iliweza kutangamana na lugha ngeni zilizotumika katika shughuli anuwalii za kiutawala. Ni kutokana na sababu hii majina ya kigeni yaliweza kuingia katika jamii ya Wakuria.

#### 4.2.10. Dini ya Magharibi

Kabla ya majilio ya dini za kimaghari, Wakuria walikuwa na dini yao na bado ingali sehemu ya maisha yao na tajiriba ya kuishi siku hadi siku. Kwa sababu hiyo bado ni vigumu kutengwa na maadili yaliyotarajiwu yazingatiwe maishani. Wakuria walimfahamu na kumwamini Mungu Muumba wa vituv yote. Kwa kuwa yeye ndiye muumba, waliamini kuwa aliquwa na uwezo wa kuwapa watu uzima, utajiri, mazao, uza, mvuanahataupepo. Kwa namna nyininge, waliamini kuwa neema na laana hutoka kwa Mungu.

Imani kama hii iliwapalekeea Wakuria kushikilia dhana ama imani ya majaliwa. Ilikuwa ni rahisi kwao kukubali hali zao. Iwapo msimu fulani haukuwa mzuri kwa mimea yao na hivyo kupata mazao duni, waliikubali hali hiyo kama mapenzi ya Mungu ingawa kwa kawaida walifanya kafara kama ishara ya kuomba toba kwa Mungu wao. Wakuria walimsifu Mungu kwa kumwita majina mengi kama; enokwi, gekoni, geteemi, mosachaobiaro, keng'ori, nyamohanganarioba.

Majina haya huonyesha utukufu wa Mungu kama Muumba, mgawaji wa neema, baraka na uwezo wa kugeuza mambo katika hali fulani. Sifa hizi zote

ziliwafanya Wakuria kuamini kuwa kiburi cha mtu kujivunia uzima, uzazi, utajiri au hali yoyote ile kungesababisha hasira ya Mungu Muumba, akampiga na kumnyang'anya neema aliyonayo tayari. Kwa sababu hii Wakuria walionya wasijivunie chochote walichonacho. Dini ya Wakuria ilishabihiana na ya jamii ya Igbo nchini Nigeria. Jamii ya Igbo iliamini katika Kiumbe Mkoo aliyeudhibiti ulimwengu na vyote vilivyomo ([Chukwuma na wenzake, 2017](#)). Imani hii inaashiriwa na majina waliopewa wototo kama vile Chukwuemeka (Mungu ametenda mengi), Chukwuka (Mungu ni Mkoo) na Chukwuma (Mungu anajua).

Ukweli huu kuhusu Mungu wa Wakuria ulizua miiko iliyotawala mahusiano baina ya watu katika jamii. Kijinsia wanawake walihimizwa kuwaheshimu wanaume ambao iliaminika wangeweza kumlaani mwanamke hata asipate mtoto maishani mwake. Wasailiwa waliweza kutoa mifano hai ya wanawake ambao hawakuweza kupata mtoto na wengine ambao walitalikiwa na hawakuweza kuoleka tena kwa sababu ya kuwatusi waumeza. Wanaume walikuwa na nguvu katika jamii, aidha walitumia vitisho vingi ambavyo vilifungamana na imani kwamba kwa ajili yao, Mungu atakuwa radhi kuwalaani wasichana wanaokataa kuwapenda wanaume husika. Kupendwa kwa mwanamume ili kuwa kama haki ya kuzaliwa, hawakutarajia kukataliwa na mwanamke yeote.

Wakuria pia waliabudua bhakoro (wafu). Jamii hii iliamini kuwa mtu akifa hugeuka na kuwa kiumbe kingine kama nyoka au mdudu au mnyama. Viumbe hawa huitwa abhakoro. Hawa, ilielezwu kuwa, wangeweza kuwaletea shida au baraka kutegemea matendo na mahusiano yao na binadamu. Wakuria walijua kwamba daima Mungu ni mtakatifu. Kwa hivyo, ibada zao zilitayarishwa vilivyo. Watu walijitakasa kwa kuacha kutenda mambo fulani. Mathalan, waliacha kujamiihana, kulimama shamba, kukata au kuchuma mimea.

Dini hii ya Wakuria bado ingalipo japo ile ya kimagharibi imeipiku. Hii ni kwa sababu kwenye karne ya sasa Wakuria wengi wameegemea sana ukristo. Hata hivyo, kuna baadhi, ambao si wakristo lakini hujihusisha na shughuli mbalimbali za kikritona pia hujaribu sana kuishi na kutenda kwa kuzingatia matakwa na misingi ya ukristo. Kwa sababu hiyo kama wanavyooleza [Nonye na Mathias \(2018\)](#) kuhusu jamii ya Igbo, utamaduni na itikadi za kijamii taratibu huegemea upande wa itikadi za kimagharibi.

Kabla ya majilio ya dini hii ya magharibi, watoto walipewa majina kwa kuzingatia ruwaza mbalimbali zilizofungamana na mila, desturi na itikadi za jamii husika. Dini za kimagharibi zilipotia nanga katika jamii nyingi za Kiafrika, jamii ya Wakuria ikiwemo, ruwaza hizi zilibadilika. Hii ni kwa sababu mwingiliano wa lugha ya Kikuria na dini ya magharibi iliyotumia lugha ngeni ulipelekewa ukopaji wa maneno, misamiati na majina pia. Ukopaji huu ulidhihirisha kama anavyooleza [Buliba \(2010\)](#) kuwa lugha ina uhai na hukua na kubadilika. Kwamba, lugha haiwi kwenye ombwe tupu kwani hutangamana na kuathiriana na lugha nyingine. Hata

hivyo, kiwango cha kuathiriana huku hutegemea kiasi cha mwingiliano baina ya lugha zinazohusika.

Kutokana na athari ya dini ya magharibi watoto wa kisasa hawapewi majina kwa kuzingatia ruwaza zilizoongozwa na kushamirishwa na itikadi za jamii ya Wakuria. Aidha, hata yale majina aliyopewa mtoto baada ya mzazi wake kufiwa na wengine wengi ili mauti yasimfike, hayatumiki tena. Kama anavyooleza [Huckles \(1997\)](#) katika mhimiili wa kintazamo, wazazi na wanajamii kwa jumla wameweza kubaini jinsi ruwaza za ujinaishaji katika jamii ya Wakuria ni mbinu mwafaka ya kuendeleza lugha yao ambamo mmekitwa itikadi za ujinsia. Kwa minajili hii, majina ya Kikristo hutumika. Majina katika [Jed.10](#) yanaonyesha ujinaishaji mpya ambao umeghubikwa na imani, madhumuni na itikadi za kikristo.

**Jed. 10:** Majina yaliyotafsiriwa. Asili: Nyanjani, 2020

Jinsia ya Kiume	Jinsia ya Kike
Joseph	Josephine
Victor	Victoria
David	Davina
Allan	Allana
Brian	Briana

Utafiti huu ulibaini kuwa dini iliyotangulia ni ya Waroma (Wakatoliki) na Wasabato. Mbinu na tamaduni za Wakuria zilionekana kuwa za giza na hivyo kutupiliwa mbali kama walivyooleza wasailiwa. Hivyo, Wakuria walibatizwa na kupewa majina mapya na kushauriwa kuishimaisha mapya yanayoakisi mienendo na matakwa ya ukristo. Isitoshe, msailiwa mwingine alieleza kuwa wakristo hawa walipopata watoto kwa mujibu wa dini ya Katoliki walihitajika tu kuuliza siku hiyo ilikuwa ya mtakatifu yupi kisha wangempa mwana wao jina la mtakatifu huyo. Dini ya Wakatoliki wa Roma ina kamusi ya majina ya Watakatifu ([Mgulunde, 1989](#)). Waroma hawakusumbuka kutafiti historia au maadili ya mhusika huyo ikizingatiwa kuwa watakatifu wote walikuwa waadilifu. Watakatifu hawa walionyesha kuwa kuishi kikristo kunahusiana na kila tukio katika kila sehemu ya maisha ya kila siku kwa sababu maneno na matendo yote hayana budi kupatana kabisa na injili ya Bwana.

Mtoto aliyezaliwa tarehe 21 Februari alipewa jina Petro Damiano. Watarehe 7 Juni aliitwa Anna Bartolomeo, tarehe 9 Julai aliitwa Veronika Giuliani, tarehe 18 Septemba alipewa jina Yosefu wa Koperitino kwa mujibu wa kamusi ya majina ya Watakatifu. Majina haya yalitafsiriwa katika Kiswahili, lugha ambayo ilikuwa inatumika kwa upana katika jamii ya Wakuria. Iwapo jina la Mtakatifu lilitofautiana na jinsia ya mtoto, jina la siku zilizofuatia lilizingatiwa au kuangalia kinyume cha jina hilo.

Wapo Watakatifu wa Afrika vile vile. Mathalan, tarehe 5 Machi - Marko natarehe 17 Mei - Adriano wote wa kutoka Misri, Afrika kaskazini.

Kwa kuzingatia ruwaza ya ujinaishaji wa Waroma inabainika kuwa dini hii iliathiri na kubadilisha itikadi za ujinsia katika jamii ya Wakuria. Mosi, kulingana na Waroma, Watakatifu wote ni mashujaa wawe wa jinsia ya kike au ya kiume. Hii inadhihirishwa na uwepo wa

majina ya jinsia zote mbili katika kamusi ya majina ya Watakatifu. Kulingana na jamii ya Wakuria, ushujaa au ushupavu ni sifa za kiume ambazo hujenga na kuendeleza nafasi ya mamlaka na utawala wanayotunukiwa wanaume kwa misingi ya mila, desturi na itikadi za kijamii, wanawake huchukuliwa kuwa waoga ambaa siku zote wako chini ya utawala na ulinzi wa mwanaume.

Mtazamo huu wa jamii ya Wakuria unashadidia maelezo ya Wodak na Reisigl (keshatajwa) kuwa ujinaishaji si kitendo kisichopendelea upande wowote bali huakisi na kuendeleza mienendo ya kimamlaka. Kwa misingi ya itikadi za Waroma, jinsia zote mbili zilipewa nafasi sawa kwani binadamu wote ni sawa mbele za Mungu. Aidha, Waroma hawakutofautisha siku za kuwapa watoto jina kama ilivyokuwa kwa Wakuria. Jamii ya Wakuria ilimpa mtoto wa kiume jina baada ya siku nne na mtoto wa kike baada ya siku tano. Hii iliashiria kuwa kutokana na ule ushujaa anaohusishwa nao mwanamumee mtoto wa jinsia ya kiume alipona haraka akilinganishwa na mtoto wa jinsia ya kike.

Kulingana na Wasabato, wasailiwa walieleza kuwa watoto walipewa majina baada ya siku nane tangu kuzaliwa awe wa jinsia ya kike au kiume. Majina yao yalitolewa kwenye Bibilia. Majina yaliyoteuliwa ni ya watu waliokuwa waadilifu. Mathalani, Abeli, Enoka, Kalebu, Daudi, Ezekiel, Samwel, Danieli, Fanueli, Musa, Yakobo, Paulo, Yoeli, Maria, Esta, Ruth, Naomi, Tabitha, Debora, Martha, Mariamuna Rahab. Kwa sababu hii, majina yaliyoendeleza itikadi za Kikuria yametelekezwa na mahali pake kuchukuliwa na ya Kikristo. Mathalan, wazazi waliofiwa na watoto wao au kuchukua muda mrefu, walipobarikiwa kwa kupata mtoto, majina kama vile: Baraka, Neema, Zawadi, Bahati na Furaha yalitumiwa kinyume na majina yaliyopendelekezwa kiitikadi kama vile Nyamboto na Kibondora. Waliobatizwa walidondosha majina yao ya kiasili na kubaki na lile la kikristo hata kwenye kitambulisho. Mfano, yupo Msailiwa alisema kuwa yeye alidondosha jina lake la asili akabaki na la kikristo na lile la baba yake na ndivyo ilivy kwenye kitambulisho cha taifa na yeti vyake vyote.

Kilichobainika kutokana na utafiti huu ni kuwa wamisheni walitumia lugha ya Kiswahili kwa upana katika kueneza dini yao. Wasailiwa walieleza kuwa vitabu vitakatifu kama vile Bibilia na nyimbo takatifu zilikuwa katika lugha ya Kiswahili. Ni katika vitabu hivi ambapo majina ya Kiswahili yalitolewa kumpa mtoto au mtu anapobatizwa. Aidha, inadhihirika kama wanavyosema Wodak na Reisigl (keshatajwa) kuwa, majina hufichua jinsi lugha huakisi na vilevile kuumba hualisia wa kijamii. Hata hivyo, ni muhimu kutaja kuwa utafiti ulibaini kuwa pamoja na mabadiliko haya ya kidini, kisiasa na kielimu, lile jina la kiasili (Kikuria) analopewa mtoto bado huwa lina minong'ono yenye nguvu ambazo zinapiku usasa uliopo.

## 5. Hitimisho

Ujio wa elimu na dini umekuwa na mchango mkubwa katika kubadilisha itikadi za ujinaishaji katika jamii ya Wakuria. Utafiti huu ulibaini kuwa dini ya magharibi ndio ilikuwa ya kwanza katika kubadilisha itikadi hizi za

ujinaishaji katika jamii ya Wakuria. Dini hii ilitumia lugha ya Kiswahili na iliathiri ruwaza za ujinaishaji. Jamii ya Wakuria ilipokea majina mengi ya kigeni yaliyohusishwa na dini ya Kikristo kama vile Yusufu, Ezekiel, Mariamu, Samwelina Yohana.

Elimu ya magharibi vilevile imekuwa na mchango mkubwa. Wakuria walikuwa na elimu yao ya kijadi iliyoza na kushamirisha itikadi zilizoiongoza jamii yao. Majilio ya elimu ya magharibi yalileta mchomozo wa itikadi ngeni. Wanajamii wengi walifupisha majina yao, wengine wakapendelea majina ya wasomi na watu maarufu na wengine walipata majina yao kwa kutumia utandawazi. Utafiti wetu ulibaini kuwa Wakuria waliochukua majina yasiyo ya asili hawakutaka kujihusisha na itikadi ambazo kwao zilikuwa ama zimepitwa na wakati, zilihusiana na maisha ya giza au zilikuwa kandamizaji.

Katika utafiti huu, ilibainika kuwa wanawake ndio waligugumia mabadiliko haya. Hata hivyo ni muhimu kutaja kuwa jina lile la asili analopewa mtoto ilibainika kuwa lina minong'ono yenye nguvu zinazopiku usasa uliopo. Suala jingine lililojitekeza ni kuwa majina mengi yaliyochomozwa na dini na elimu yalikuwa ya Kiswahili jambo ambalo lisaidia katika kuendeleza na kusambaza lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wakuria. Isitoshe, majina mengi hayakutokana na elimu na dini tu bali matumizi ya utandawazi.

## Marejeleo

Allagbe, A. A (2016). Character Naming and Authorial Attitudes in Contemporary African Literature. In Research on Humanities and Social Sciences Vol.6, No.4

Buliba, A. (2010). Fonolojia Tohozi. Kiingereza - Kiswahili. Division of Research and Extension 2010. Egerton University.

Chukwuma, O. K na Wenzake. (2017). Conflicts Between African Traditional Religion and Christianity in Eastern Nigeria. The Igbo Example. SAGE Open April-June 2017: 1-10.

Djik, A.T. (2001). Multidisciplinary CDA; A plea for Diversity. In Ruth Wodak and Meyer (Eds) Methods of Critical Discourse Analysis. London: Sage pg. 55 - 120

Essien, O. E. (1986). Ibibio Names, Their Structure and Their Meanings. Ibadan: Daystar Press.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). Misingi ya Sarufi ya Kiswahili. Nairobi: Phoenix Publishers.

Holmes, J. & Meyerhoff, M. (2003). The Handbook of Language and Gender, First Edition. USA: Blackwell Publishing Ltd.

Huckins, T.N. (1997). Critical Discourse Analysis. Toronto. University of Toronto Press.

Kjerland, K. (1995). Cattle Breed, Shillings Don't: The Belated Incorporation of the Abakuria into Modern Kenya, PhD Dissertation, University of Bergen.

- Macheba, M. (2002). Naming, heritage and identity in post apartheid South Africa. Paper read at the International Congress for names. University of the Free State 27-29 May 2002.
- Kihore, Y.M., Massamba, D. P. B., Msanjila Y. P. (2010). Sarufi Maumbo Ya Kiswahili Sanifu. Taasisi Ya Uchunguzi wa Kiswahili Dar es Salaam.
- Mgulunde, M. (1989). Maisha ya Watakatifu. Tabora. TMP Book.
- Moyo, T. (1996). Personal Names and Naming Practices in Northern Malawi. *Nomina Africana*. 10 (1 - 2). 47 - 57.
- Mweri, G. (2010). Utangulizi wa Isimu. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Mwita, B. M. (2005). "Dhima ya Ichingero za Wakuria Kusawiri Taswira yaMwanamke."Tasnifu ya Ph.D Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.
- Nonye, O.B. & Mathias, B. A. (2018). Igbo Cultural Naming Patterns and Western Religion in Selected Communities in Awka-South Anambra State South Eastern Nigeria. Mnadi Azikiwe University, Awka Journal of Sociology. Vol. 6 No.1 April 2018.
- Rossiland, F. (1990). Marxism and Ideology. Oxford: Clarendon Press.
- Tibezuka B. C., Akaka, L. na Maithya, J. (2021). Mabadiliko Katika Uteuzi wa Majina ya Koo Miiongoni mwa Wazinza Nchini Tanzania. Editon Cons. J.
- Wodak, R. & Reisigl, M. (2001). Discourse and Discrimination: Rhetorics of Racism and Ati-Semitism. London: Routledge.